

Sababu za matumizi ya dawa za kulevya

By SW - Melkisedeck Shine · April 17, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngoni Salama

Zipo sababu nyingi zinazowafanya watu kutumia dawa za kulevya, nazo ni kama zifuatazo: Watu wengi hutumia dawa wakitumaini kusahau matatizo yanayowakabili, wengine hutumia kama viburudisho na wanataka kujionyesha kwamba ni watu wazima na wenye nguvu. Wengine pia huanza kutumia dawa kiutani na hatimaye hushindwa kujizuia kuzitumia. Wengine hutumia kutokana na msukumo wa rika au kutokana na kushawishiwa na watu wengine kwamba dawa za kulevya huwapa raha. Wengine hutumia kutokana na ukali wa maisha, uchovu pamoja na upweke. Kimsingi, dawa za kulevya hazimpatii mtu ufumbuzi wa matatizo, bali humwongezea matatizo mtumiaji.

Printable AckySHINE Article · <https://ackyshine.com/post.php?post=25779>